Unyanyasaji wa watoto ni nini?

Kijitabu cha kuelimisha katika kampeni ya "*Tulinde watoto sasa!*"

sasa.mkombozi.org

yaliyomo

1. Utangulizi uk.4

1.1 Kwa nini ni muhimu kujifunza kuhusu unyanyasaji wa watoto? *4*
1.2 Istilahi na maana *6*

2. Unyanyasaji wa watoto ukoje? uk.8

2.1 Unyanyasaji wa watoto unatokea vipi na nini chanzo chake? *8*

3. Unyanyasaji wa watoto hutokea wapi? uk.12

4. Madhara ya unyanyasaji wa watoto ni yapi? uk.16

4.1 Madhara ni zaidi ya kile ambacho macho yanaweza kuona *16*
4.2 Unyanyasaji wa watoto una madhara kijamii na kiuchumi *18*
4.3 Unamtambuaje mtoto aliyenyanyaswa - dalili ni zipi? *20*
4.4 Unyanyasaji unawafundisha watoto nini? *21*

*"**Tulinde Watoto Sasa!**" (Kiswahili for "**Let's Protect Children Now!**") ini kempeni ya kuinua ufahamu ambayo huelimisha sehemu kubwa ya raia wa Tanzania kuhusu madhara ya unyanyasaji watoto.*

"Hakuna unyanyasaji wa watoto unaokubalika, na unyanyasaji wo wote wa watoto unazuilika."

UN Secretary-General study on violence against children

Dhumuni la kijitabu hiki ni nini?

Kijitabu hiki ni kwa ajili yako...

WEWE ni mtu unayehusika na watoto kwa namna yoyote ile.

WEWE ni mama, baba, kaka, dada, ndugu, mwalimu, kiongozi katika jamii, daktari, kiongozi wa dini, afisa polisi, mfanyakazi wa idara ya ustawi wa jamii, mwanajamii, rafiki wa mtoto, dereva wa basi la shule, mlinzi… au wewe mwenyewe unaweza kuwa mtoto.

Kitabu hiki kina lengo la kukuelimisha kuhusu unyanyasaji wa watoto - mazingira ambapo unatokea, wapi na vipi unyanyasaji unafanyika, na kuhusu madhara yake. Kwanini? Kukutia wewe msukumo ili uwalinde watoto!

Unaweza kujifunza zaidi >>> ***www.sasa.mkombozi.org***

1. utangulizi

1.1 Kwa nini ni muhimu kujifunza kuhusu unyanyasaji wa watoto?

Sasa ni wazi kwamba unyanyasaji wa watoto una madhara…

Watoto wamekuwa wakiteseka na unyanyasaji unaofanywa na watu wazima kwa miaka mingi sasa, na unyanyasaji kwa kweli sasa si jambo jipya. Hata hivyo, kwa sasa tafiti katika eneo hili zinaipatia dunia ushahidi kuhusu madhara yake. Katika utafiti wa Umoja wa Mataifa kuhusu unyanyasaji wa watoto imeandikwa "ingawa unyanyasaji wa watoto umeenea sana, unazuilika, na dunia inazo rasilimali za kuutokomeza".

Ukimya lazima uvunjwe…

Unyanyasaji sio asili na wala sio lazima katika maisha ya watoto, na kwa hivyo tusiukubali. Kama tunataka kuona mabadiliko - katika sheria, katika jamii, katika familia, katika huduma, katika taasisi na mashirika - ni lazima kwanza tutambue upana wa hili tatizo. Tunachoweza kufanya ni kuliweka wazi - kuanza kwa kuliongelea.

Uelewa kuhusu unyanyasaji unawapa watu nguvu ya kuuzuia...

Ni kweli kwamba, jamii yetu tangu muda mrefu sasa imekuwa katika hitaji kubwa la kupata sheria za kuwalinda watoto. Lakini, kutokomeza unyanyasaji wa watoto sio mchakato wenye lengo la kuwatia hatiani wanaohusika tu. Kutokomeza unyanyasaji wa watoto ni mchakato wa utoaji elimu kwa watu wote na wadau wote katika jamii yetu yote. Bila kuongeza uelewa, ubadilishaji wa tabia na ufumbuzi ulio mpana na wa kudumu utakuwa mgumu kupatikana. Unyanyasaji wa watoto lazima ujadiliwe katika kila Mkoa, mji na kijiji katika nchi yetu.

Kutokomeza unyanyasaji kunalinda maslahi ya watoto wetu leo...

Watoto wanayo haki ya maisha ya utoto yasiyo na unyanyasaji. Hata hivyo, haki za watoto zinavunjwa kila siku. Tunaona umuhimu wa haraka kusimamisha namna zote za unyanyasaji wa watoto kwa sababu unaathiri afya zao, ustawi na hata fursa mbalimbali katika maisha yao ya baadaye. Kampeni ya Tulinde watoto sasa! inatetea haki za watoto ambao wananyanyasika leo. Tunakataa unyanyasaji, na tunautia moyo umma kuingilia kati unapoona mtoto ananyanyaswa.

Kulindwa ni haki ya kila mtoto. Kuwalinda watoto ni jukumu la kila mtu!

Jamii nzima inaweza kufaidika...

Kwa kufanya kazi kupunguza unyanyasaji wa watoto, tunachangia kupunguza unyanyasaji kwa wote - vijana na wazee - katika jamii zetu. Kuvunja mzunguko wa unyanyasaji kunaweza kujenga jamii yenye amani zaidi ambayo matendo ya unyanyasaji siyo sehemu asilia ya utatuzi wa migogoro. Kama sehemu ya dhamira ya tulinde watoto sasa!, tunaona kwamba kuwekeza katika vijana na watoto kuna uwezekano mkubwa kuifaidia jamii kwa ujumla.

Kazi yetu inalenga kutokomeza unyanyasaji…

Kampeni ya tulinde watoto sasa! inalenga kuboresha ufahamu wa umma juu ya mzigo wa kijamii ambao ni matokeo ya kuwanyanyasa watoto. Tunaamini kwamba endapo watu watafahamu vema madhara ya unyanyasaji katika maisha ya watoto, vivyo hivyo na kufahamu vema faida kuu za kuwalinda watoto, hii inaweza kuleta msukumo na chachu ya kujenga jamii salama na inayojali watoto. Mkombozi inajitahidi kuibua changamoto na kushawishi kuwepo kwa badiliko katika desturi za kijamii na tamaduni ambazo huhalalisha na kukubalina na unyanyasaji wa watoto.

1.2 Istilahi na maana...

Unyanyasaji wa watoto, udhalilishaji wa watoto, uonevu wa watoto, ukatili na kutelekeza watoto - maneno haya yote na mengine kama haya yanazungumzia kitu kimoja. Maneno haya yote yanaelezea vitendo vinavyoweza kumdhuru mtoto. Kwa mujibu wa katiba ya jamhuri ya mungano ya Tanzania, mtoto ni mtu mwenye umri chini ya miaka 18.

Maana ya "unyanyasaji wa watoto" ni nini?

Ni vitendo au maneno, ambavyo vimekusudiwa dhidi ya mtoto au vikundi vya watoto na vinaweza kusababisha madhara ya kiafya, kimaendeleo, makuzi au utu - bila kujali dhumuni la vitendo au maneno hayo.

"Madhara" inamaanisha nini?

- Ni pale ambapo afya ya mtoto kiakili, kimwili, kihisia na kijinsi imedhurika.
- Ni pale ambapo maendeleo ya mtoto yanavurugwa.
- Ni pale ambapo uhai wa mtoto uko hatarini.
- Ni pale ambapo utu wa mtoto unapodhurika.

Nini kinatofautisha unyanyasaji wa watoto na unyanyasaji wa watu wazima?

Kwa ujumla watu wazima wana nguvu na mamlaka zaidi ukilinganisha na watoto. Hili linafanya watoto washindwe kuzuia unyanyasaji dhidi yao, hasa pale ambapo anayewanyanyasa ni mlezi wao. Tunaweza kusema kwamba watoto ni viumbe dhaifu kimwili, kihisia na kisaikologia ukilinganisha na watu wazima. Hii ni kwa sababu akili zao na miili yao iko katika hatua za ukuwaji. Kinachotokea katika kipindi cha ukuwaji wa watoto kinaathiri afya na tabia - sasa na hata baadaye wakiwa watu wazima. Kwa maana hiyo, mtoto aliyenyanyaswa yuko hatarini zaidi kuathirika kiakili, kimwili na kisaikologia katika maisha yake yote.

Nini tofauti kati ya adhabu ya viboko na unyanyasaji?

Jibu ni kwamba hakuna tofauti. Adhabu ya viboko, hata ikiwa ndogo kiasi gani, ni unyanyasaji. Kwanini? Kwa sababu hata ikiwa kwa kiasi kidogo, inaweza kumdhuru mtoto. Inatupasa tujiulize: Lengo la kutumia adhabu ya viboko ni nini? Unajenga mazingira gani kati yako na mtoto? Je, kuna matokeo tusiyoyataka na tusiyoyatarajia? Je, tunatumia adhabu ya viboko kuwafundisha watoto tabia njema? Hata kama lengo ni kurekibisha tabia zao, inaweza kusababisha madhara katika maisha yao yote. Utafiti unaonyesha kwamba, hata kama adhabu ya viboko ni kidogo, inaweza kumdhuru mtoto kimwili, kiakili au kiroho. Kijitabu hiki kinaonyesha madhara na matokeo ya unyanyasaji wa watoto.

unajua kwamba? **Hapa Tanzania mfumo wa sheria kuhusu watoto umekuwa haujitoshelezi na una mapungufu. Hata hivyo, kwa sasa Tanzania inapiga hatua katika masuala yahusuyo haki za watoto kwa kujihusisha kufanya mabadliko katika sheria zinazowahusu watoto. Kwa kuridhia Azimio la Haki za Mtoto (Convention on the Rights of the Child, CRC) taifa limekubali kuboresha mfumo wa sheria kuhusu watoto kukubaliana na viwango vya kimataifa kama ilivyoelezwa katika CRC.**

Azimio la Haki za Mtoto

Azimio la Haki za Mtoto (Convention on the Rights of the Child, CRC) ni chombo cha kimataifa kuhusu haki za mtoto chenye lengo la kuimarisha haki za mtoto katika kila pembe ya dunia - ikiwemo Tanzania.

Kifungu 3(1): Katika vitendo vyote vinavyofanywa kuhusu watoto, viwe vimefanywa na taasisi za ustawi wa jamii zinazoendeshwa na umma au binafsi, mahakama, mamlaka za utawala au vyombo vya kutunga sheria, maslahi ya mtoto yapewe umuhimu wa kwanza.

Kifungu 6: Serikali zinatakiwa kuhakikisha kwamba kila mtoto ana haki ya msingi ya kuishi, na kwa kiwango cha juu kiwezekanacho, uhai na maendeleo.

Kifungu 12(1): Nchi wanachama zitamhakikishia mtoto mwenye uwezo wa kutoa maoni yake haki ya kutoa maoni hayo kwa uhuru katika maswala yote yanayomhusu, na mawazo ya mtoto yatapewa uzito unaostahili kulingana na ukomavu wake.

Kifungu 19(1): Nchi wanachama zitachukua hatua zote zinazofaa za kisheria, kitawala, kijamii na kielimu katika kumlinda mtoto dhidi ya aina zote za ukatili, kudhurika au kunyanyaswa, kutelekezwa au kutojaliwa, kutendwa visivyo au kunyonywa, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kingono, wakati akiwa katika malezi ya wazazi, walezi wa kisheria au mtu mwingine yeyote anayemtunza mtoto.

Kifungu 34: Serikali zinatakiwa kumlinda mtoto kutokana na aina zote za unyonyaji na unyanyasaji wa kingono na kuchukua hatua zote zinazofaa kuzuia, pamoja na mambo mengine, kumshawishi au kumlazimisha mtoto kufanya ngono isiyo halali.

2. unyanyasaji ukoje?

2.1 Unyanyasaji wa watoto ukoje na unatokea vipi?

Kuna aina tatu za unyanyasaji: **1.** Unyanyasaji unaojifanyia mwenyewe (kujinyanyasa mwenyewe); **2.** Unyanyasaji dhidi ya mtu mwingine; **3.** Unyanyasaji dhidi ya vikundi vya watu. Katika kijitabu hiki tunaongelea aina ya pili ya unyanyasaji - **unyanyasaji dhidi ya mtu mwingine**. Aina hii inajumuisha unyanyasaji katika familia, katika jamii, kati ya vijana wenyewe kwa wenyewe, na hasa watoto kunyanyaswa na watu wengine.

Unyanyasaji wa kimwili…

Unyanyasaji wa kimwili ni vitendo ambavyo vinaweza kusababisha madhara ya kimwili kwa mtoto, na inaweza hata kusababisha kifo. Aina hii ya unyanyasaji wa watoto mara nyingi inatumika kama adhabu inayolenga kuleta maumivu au kero.

Hii ni mifano ya unyanyasaji wa kimwili: ▶ Kumpiga ▶ Kumpiga kibao ▶ Kumpiga teke ▶ Kumtikisa ▶ Kumng'ata ▶ Kumkaba ▶ Kumkata ▶ Kumchoma ▶ Kumchapa ▶ Kumpa sumu ▶ Kumkosesha pumzi ▶ Kumfinya ▶ Kumfinya masikio ▶ Kumrusha kichura ▶ Kumvuta nywele ▶ Kumlazimisha kula kitu ▶ Kumfunga na kamba ▶ Kumparua ▶ Kupiga kwenzi ▶ Kumninginiza ▶ Kumdhuru kwa kutumia silaha ▶ Kumsukuma ▶ Kumchapa mijeledi ▶ Kumburuza ▶ Kumpa adhabu za kazi zilizozidi uwezo wake

unajua kwamba? Kati ya nchi ambazo World Health Organisation (WHO) linafanya kazi, **kiwango cha juu cha mauaji ya watoto** chini ya miaka 5 yanatokea katika ukanda wa Afrika; **17.9 katika kila 100,000 kwa wavulana, na 12.7 katika kila 100,000 kwa wasichana**. Ukweli, katika nchi nyingi watoto wanaotoka katika familia duni wana uwezekano wa kupata adhabu za kikatili sawa na wale wanaotoka katika familia za kitajiri. Pia watoto wanaoishi mazingira ya vijijini wana uwezekano wa kunyanyaswa kama watoto waishio katika mazingira ya mji. Utafiti wa United Nations Children's Fund (UNICEF) kutoka nchi 29 unaonyesha kwamba **asilimia 86 ya watoto** wenye umri kati 2-14 **wamewahi kupata adhabu za kinyanyasaji nyumbani.** (Source: UNICEF 2007)

“Huna haki ya kuongea,
unajisikia vibaya sana,
unakosa amani kwa kweli.”

Mazungumzo ya Msichana kuhusu jinsi kupigwa kulivyo

Unyanyasaji wa kingono...

Unyanyasaji wa kingono unatokea pale ambapo mtu amejihusisha katika vitendo vyovyote vya ngono na mtoto. Hata kama mtoto anaonekana kukubali kufanya vitendo hivi, hili litaonekana kuwa unyanyasaji wa kingono kwa sababu mtoto hana ufahamu wa kutosha, hivyo hawezi kuridhia. Hata hivyo maumbile ya mtoto hayako tayari kwa vitendo vya ngono. Watoto wanaweza kunyanyaswa kingono na watu wazima au na watoto wenzao wa rika moja. Katika unyanyasaji wa kingono, mtu anamtumia mtoto ili kujiridhisha.

Hii ni mifano ya unyanyasaji wa kingono dhidi ya watoto: ▶ Kumvua nguo au kumbusu kwa lengo la kumfanyia vitendo vya ngono ▶ Kujamiana au kumbaka ▶ Kumpapasa ▶ Kumtongoza ▶ Kumpiga picha za ngono au kumuonyesha picha za ngono ▶ Kumkonyeza

unajua kwamba?

Wasichana kuolewa mapema - **ndoa za utotoni** - ina madhara makubwa sana kwa afya zao, maendeleo na haki. Mara nyingi inawaondolea fursa ya kupata elimu na matokeo yake ni kutengwa kijamii. Wake vijana katika ndoa za utotoni wanapata kwa kiwango kikubwa matatizo katika kujifungua na vifo vinavyohusiana na uzazi. Taarifa zilizokusanywa kati ya 1996 - 2003 na UNICEF zinaonesha **kwamba 39% ya wasichana wa kitanzania** walikuwa wameshaolewa walipofikia umri wa **miaka 18**.

unyanyasaji ukoje?

Unyanyasaji wa kisaikologia au kihisia…

Katika aina hii ya unyanyasaji, mtoto hufanyiwa vitendo ambavyo vinaweza kumdhuru kihisia na kisaikologia. Unyanyasaji huo unaweza ukawa kwa njia ya vitendo, maneno au tabia.

Hii ni mifano ya unyanyasaji wa kisaikologia au kihisia dhidi ya watoto: ▶ Kumdharau: "Toka hapa!" ▶ Kumlaumu: "Unakula sana, utanifilisi!" ▶ Kumtishia: "Nikikukamata nitakumaliza!" ▶ Kumwita majina: "Wewe mjinga!" ▶ Kumbagua (mfano: unawapendelea watoto wako kuliko mtoto wa kambo) ▶ Kumkataa (mfano: kufanya vitendo vinavyo onyesha humhitaji mtoto) ▶ Kumtukana / kutumia lugha ya matusi: "Mzembe kama shangazi yako!" ▶ Kuwa mkali kupita kiasi kwa mtoto

Kutelekeza…

Kutelekeza kunatokea pale ambapo mzazi au mlezi hampi mtoto huduma ambazo ni muhimu kwa maendeleo yake, hata kama ana uwezo wa kumpa huduma hizo, na ana ufahamu wa umuhimu wa hizo huduma. Pia, hutokea pale ambapo mzazi au mlezi anashindwa kumlinda mtoto dhidi ya hatari. Kutelekeza kunaweza kutokea katika maeneo matano yafuatayo:

- AFYA: Kutokufuatisha kanuni za afya, au kutompa mtoto matibabu.
- ELIMU: Kutokufuatilia maendeleo ya shule ya mtoto, au kutomwandikisha shule.
- MAENDELEO YA KIHISIA: Kutokuzingatia hisia za mtoto.
- LISHE: Kumnyima mtoto chakula, au kutompa lishe bora.
- MAKAZI SALAMA: Kutohakikisha mtoto anaishi katika mazingira salama, na hivyo kumfanya awe katika mazingira hatarishi.

"Kama mtu anakutukana unajisikia vibaya sana. Wananiona kama mimi si binadamu. Kama mimi ni mbwa."

Mvulana kuhusu kutukanwa mitaani

"Nilipokuwa nimemaliza shule ya msingi, hawakutaka kunisomesha tena. Mama mkubwa alikuwa hanitaki."

Mama kijana kuhusu utoto wake

Mila na desturi potofu…

Vitendo vya tamaduni nyingine vinasababisha maumivu na vinaharibu maumbile ya mtoto. Ingawa vitendo hivyo vina maana na umuhimu katika tamaduni hizo, vinadhuru watoto.

Hii ni mifano ya vitendo hivyo ▶ Kumchanja mtoto chale ▶ Kumkeketa

Kushuhudia vitendo vya unyanyasaji…

Mara nyingi watoto wanashuhudia vitendo vya unyanyasaji nyumbani, kwa mfano kusikia au kuona ugomvi wa wazazi au watu wengine. Kushuhudia vitendo vya unyanyasaji vinamdhuru mtoto hasa pale ambapo anayenyanyaswa / anayenyanyasa ni mtu ambaye ana mahusiano naye ya karibu.

Ifuatayo ni mifano ya kumfanya mtoto ashuhudie unyanyasaji: ▶ Baba kumpiga mama mbele ya mtoto ▶ Baba na mama wanagombana mbele ya mtoto ▶ Mlezi kulewa na kutukana mbele ya mtoto

ni kweli kwamba...

Taarifa zilizokusanywa 1996-2004 zinaonyesha kwamba 18% ya wanawake wa Tanzania wenye umri kati ya 15-49 walikuwa wamefanyiwa ukeketaji.
(Source: UNICEF 2005)

pia ni kweli kwamba...

Unyanyasaji unaotendeka majumbani hauathiri tu wanawake wanaonyanyaswa na waume zao, lakini unawaathiri pia watoto ambao aidha wanafanyiwa au wanashuhudia ukifanyika. Kwa kweli, afya ya watoto, ustawi wao, lishe na elimu vinawekwa hatarini. Hata hivyo tafiti za familia zilizofanywa na UNICEF zinaonyesha kwamba 60% ya wanawake na wasichana wenye umri kati ya 15 - 49 wa kitanzania wanaunga mkono mtazamo kwamba mume au mwenza ana haki kumchapa au kumpiga mkewe katika mazingira fulani fulani.
(Source: UNICEF 2007)

3. unyanyasaji hutokea wapi?

Nyumbani - kwenye familia…

Familia zina uwezo mkubwa wa kulinda watoto dhidi ya hatari na pia kuwafundisha jinsi ya kujilinda. Kwa upande mwingine, familia inaweza kuwa hatari, hasa kwa watoto wadogo kama itawanyanyasa badala ya kuwalinda. Kwa kuwa muda mwingi watoto wadogo wanakuwa nyumbani na familia zao, wako hatarini zaidi kunyanyaswa na wanafamilia kuliko watoto wakubwa. Kwa mfano, mvulana mmoja anakumbuka utoto wake ifuatavyo:

"Nilipopigwa, nilikuwa na wasiwasi sana. Niliposikia mtu anaimba, nilijua kwamba baba amerudi, na amelewa. Kawaida yake aliuliza; mtoto yuko wapi? Hapo nilijua kwamba leo nitapigwa. Nilipata wasiwasi sana, nilijiskia vibaya. Nilikuwa nafikiria kwamba aje mtu kunichukua nikaishi na familia yake. Kitu kama hiki kikitokea kwako, utajisikia vibaya na utakimbia kutoka katika hali hii na kwenda kuishi sehemu nyingine ambako utajisikia furaha."

Shuleni…

Muda mwingi, watoto wanaosoma huwa shuleni kuliko sehemu nyingine yoyote mbali na nyumbani. Wanaosimamia, ajiri na kuongoza shule wanayo mamlaka ya kuzingatia kwamba mazingira ya shule ni salama kwa maendeleo na makuzi ya mtoto. Uongozi wa shule unajukumu la kuwasaidia watoto kuwa na tabia nzuri na heshima, na sio kuwa wanyanyasaji. Hata hivyo, mazingira ya shule yanaweza kuwa chanzo cha madhara kama wanaopaswa kufundisha na kulinda watoto ndio wanaowanyanyasa. Kwa mfano, mashuleni ni kawaida kutumia adhabu ya kiboko - adhabu ambayo inaweza kumdhuru mtoto ingawa inalenga kuadabisha.

unajua kwamba? **Tisa kati ya shule kumi za majaribio katika utafiti uliofanyika Tanzania, "Maoni ya watoto 2007", watoto walielezea hofu ya kupigwa na walimu wao. Katika shule tatu walisema kwamba mwalimu anayeingia darasani akibeba fimbo "anawaogopesha watoto". Watoto walielezea kwamba hawawezi kujifunza kutoka mwalimu, au kumuelewa mwalimu, katika mazingira ya hofu. Hata kama hawapigwi, kumwona tu mwalimu amebeba fimbo inajenga hofu. (Source: Jamhuri ya Muungano ya Tanzania 2008)**

"Mimi naona wazazi hawaogopi kumvunja moyo mtoto."

Kijana kuhusu unyanyasaji nyumbani

Katika jamii…

Maana ya jamii inaweza kuwa ni eneo la kigeographia au ni kikundi cha watu. Hamna jamii isiyokuwa na vitendo vya unyanyasaji kabisa. Jamii zinatofautiana; zingine zina utulivu na zinajali wakati zingine zina kiwango kikubwa cha unyanyasaji, na hivyo kuwaweka watoto hatarini.

Watoto wanapofikisha umri fulani, hujihusisha na wanajamii, mfano: wanapanda basi kwenda shule, wanatumwa dukani au kwenda kucheza na marafiki zao. Mtoto anapotoka mwenyewe bila uangalizi, anakuwa hatarini kunyanyaswa na watu wazima au watoto wenzake. Kwa upande mwingine, jamii inaweza kulinda na kujali, na kutegemewa kuzuia unyanyasaji wa watoto.

unajua kwamba? **Adhabu za viboko mashuleni hairuhusiwi katika zaidi ya nusu ya nchi zote duniani. Kwa kweli, Ethiopia, Kenya, South Africa, Zimbabwe and Trinidad and Tobago wote wamepiga marufuku adhabu za viboko mashuleni. (Source: Global initiative to end all corporal punishment of children 2002)**

unyanyasaji hutokea wapi?

Vituo vya watoto na vyombo vya sheria…

Watoto wengine wanalelewa kwenye vituo vya watoto au vyombo vya sheria. Hivi vinaweza kujumuisha: vituo vya watoto yatima, hospitali za ugonjwa wa akili, mahabusu ya watoto, vituo vya polisi, vituo vya watoto watukutu na shule za bweni. Vituo hivi vinaweza kumilikiwa na serekali, watu binafsi, mashirika yasiokuwa ya kiserekali, makampuni na mashirika ya kidini.

Kwanza, watoto wanaoishi katika vituo hivi hubaguliwa na jamii, kitendo ambacho kinaweza kuwadhuru kihisia na kisaikologia. Pili, watoto wanaoishi kwenye vituo ukiwalinganisha na wanaoishi kwenye familia, watoto wanaoishi kwenye vituo wako hatarini zaidi kunyanyaswa.

Kazini…

Kulingana na sheria ya Tanzania, watoto wenye umri wa miaka chini ya 15 hawatakiwi kuajiriwa kabisa - hasa mahali pa kazi ambapo wanaweza kuwa hatarini kunyanyaswa. Kama mtoto amenyanyaswa kazini, suluhisho sahihi litakuwa kumondoa mahali hapa pa kazi. Hata hivyo, ni vyema kutambua magumu ambayo watoto wengi wanapitia.

Watoto wanaajiriwa kutokana na sababu za kiuchumi, kijamii na kitamaduni ambazo ziko nje ya uwezo wao, na sababu hizo zote zinahitaji kufanyiwa kazi ili kutatua tatizo hilo. Ni kawaida sana kwa watoto kuajiriwa kama housegirl na houseboy - mazingira ambayo yanamweka hatarini kunyanyaswa na mwajiri.

Nani anaweza kumnyanyasa mtoto?

Mtu yeyote anaweza kumnyanyasa mtoto wakati wowote. Wafuatao ni mifano ya watu wanaoweza kumnyanyasa mtoto:

- Wazazi
- Walezi
- Kaka au dada
- Ndugu na jamaa
- Wafanyakazi wa nyumbani
- Walimu
- Wanafunzi wenzake
- Wafanyakazi wa shuleni (mpishi, mfanyausafi...)
- Mwalimu mkuu
- Wanajamii
- Mwajiri
- Wateja na wafanyakazi kazini
- Wafanyakazi wa umma
- Walezi na wafanyakazi katika vituo
- Wageni
- Watu wanaomfahamu
- Watu wenye mamlaka

wewe unaonaje? Ujiulize kwamba:

- **Hadi lini watoto katika taifa letu** wataendelea kunyanyasika na kuathirika?
- **Ni watoto wangapi wanaodhurika** katika taifa letu leo? **Tunaweza kufanya nini** ili kuwasaidia?

UNAWEZA KUJIFUNZA ZAIDI

sasa.mkombozi.org

4. madhara ni yapi?

4.1 Madhara ya unyanyasaji wa watoto ni zaidi ya unavyoweza kuona kwa macho...

Madhara ya unyanyasaji wa watoto ni zaidi ya unavyoweza kufikiri. Madhara mengine yanajitokeza mara moja, mengine yanadumu milele. Mengine hayajitokezi mpaka baada ya miaka kadhaa tangu kitendo cha unyanyasaji kilipotokea. Tunapotafakari madhara ya unyanyasaji wa watoto, inatupasa kufikiri kwa upana zaidi; unyanyasaji unaathiri maisha ya mtu binafsi, jamii na hata taifa kwa ujumla. Unaathiri mahusiano, afya, tabia na hata uchumi. Unyanyasaji unaweza kusababisha madhara yafuatayo.

Madhara kwa maendeleo ya mtoto…

Mtoto anapokuwa mdogo, ni kipindi cha ubongo wake kukuwa. Mtoto mdogo anapokuwa na wasiwasi, anaponyanyaswa au kutokutunzwa vyema, ukuaji wa ubongo wake unaweza kuathirika na kazi za ubongo zinaweza kubadilika. Mabadiliko hayo katika ukuwaji wa ubongo yanaweza kuathiri ukuaji wa mtoto - kiakili, kimwili na mahusiano yake na watu wengine.

Madhara kwa tabia ya mtoto (leo na wakati ujao)…

- Mtoto aliyenyanyaswa anaweza kutumia pombe au madawa ya kulevya katika utoto wake au hata baadaye katika maisha yake. Tabia hii anakuwa nayo kama jinsi ya kumudu madhara ya kisaikologia aliyopata baada ya kunyanyaswa.
- Mtoto aliyenyanyaswa anaweza kujihusisha na tabia za uharibifu, ugomvi na hatari, ambazo mara nyingi ni kinyume na sheria.
- Mtoto aliyenyanyaswa anaweza kushindwa kuwa na mahusiano mazuri na watu - katika kipindi cha utoto na utu uzima. Hili mara nyingi linatokea pale ambapo mnyanyasaji ni mtu wa karibu na mtoto.
- Mtoto aliyenyanyaswa anaweza kuwa na maendeleo mabaya shuleni.
- Mtoto aliyenyanyaswa anaweza kutaka kujidhuru au kujiua.
- Mtoto aliyenyanyaswa anaweza kuwa mkatili na kuwa hatari kwa wengine.

"Ukinyanyaswa, unafikiri... Ninaishi hapa duniani kwanini? Kwanini ninaishi?"

Mwanamke kijana kuhusu unyanyasaji aliofanyiwa utotoni

Madhara kwa afya ya mtoto - leo na wakati ujao...

Mtoto anaweza kudhurika ***kimwili***, ikiwa ni pamoja na: ▶ Kuumizwa ndani ya tumbo ▶ Kuumizwa ubongo ▶ Kupata michubuko ▶ Kuungua ▶ Kulemaa ▶ Kuvunjika viungu vya mwili ▶ Kupata vidonda ▶ Kuharibika uwezo wa kuona

Mtoto anaweza kudhurika ***kijinsia*** ikiwa ni pamoja na: ▶ Matatizo ya afya ya uzazi ▶ Kutotaka kuwa na mahusiano ya kimapenzi baadaye ▶ Magonjwa ya zinaa (ikiwemo UKIMWI) ▶ Mimba za utotoni

Mtoto anaweza kudhurika ***kisaikologia***, ikwa ni pamoja na: ▶ Kulemaa kwa uwezo wa kufikiri na kujifunza ▶ Kufadhaika na kuwa na wasiwasi ▶ Kushindwa kulala vizuri ▶ Kushindwa kula vizuri ▶ Kujisikia kama ni mkosa au kuona aibu ▶ Kutokujiamini ▶ Hyperactivity ▶ Mshituko (shock) ▶ Kupata ugonjwa kutokana na wasiwasi

Mtoto anayenyanyaswa anaweza kuugua anapokuwa mtu mzima...

Watoto wanaonyanyaswa, au watu wazima ambao walinyanyaswa walipokuwa wadogo, wanaweza kuwa na tabia hatari au zenye madhara kama vile kuvuta sigara, ngono zembe, ulevi na kutumia madawa ya kulevya. Tabia hizo zinaweza kusababisha magonjwa yanayoweza kuleta kifo badaye (mifano: saratani, ugonjwa wa mapafu, ugonjwa ya moyo, ugonjwa wa ini, VVU / Ukimwi).

4.2 Unyanyasaji wa watoto una madhara makubwa kijamii na kuchumi…

Familia: Watoto wanaonyanyaswa na wazazi au walezi mara nyingi wanamkwepa mtu anayewanyanyasa. Watoto hao wanapenda kukaa wenyewe na kuwa nje ya nyumbani muda mwingi, na mara nyingine hutoroka nyumbani na kutokurudi tena. Watoto wengine ambao wanatoroka nyumbani wanaenda kuishi mtaani ambako wanakuwa hatarini zaidi kunyanyaswa. Wengine huishia kuwa chini ya uangalizi wa watu ambao wanaweza kuwaajiri au kuwatumia kimapenzi. Kuna uwezekano wa watoto wanaokimbia manyumbani kukosa elimu, kunyanyaswa na watu mbalimbali.

Elimu: Watoto wanaonyanyaswa hawawezi kujiamini na wanakata tamaa, hasa kama wananyanyaswa nyumbani na shuleni. Inaweza kuwafanya wasiwe na maendeleo mazuri shuleni, na hata kufeli mitihani. Mara nyingine elimu yao inaathirika na hivyo kupunguza nafasi ya kuajiriwa wanapokuwa watu wazima. Adhabu ya kiboko katika mashule hufanya watoto kushindwa kujifunza na kufurahia elimu. Watoto wanaosoma shule ambapo adhabu ya kiboko inatumika sana wanaweza kuacha shule, au wanaweza kuwa na maendeleo mabaya darasani.

Unyanyasaji unaongezeka: Watoto walionyanyaswa wana uwezekano mkubwa wa kuwa wanyanyasaji katika ujana au utu uzima wao. Wanaweza kujihusisha na tabia zenye madhara kama ujambazi na uvamizi. Tabia hizo zinaweza kusababisha kukamatwa na kufungwa kwa muda mrefu na hivyo kupunguza nafasi ya kuendelea kimaisha. Pia, unyanyasaji wa watoto unaongeza wimbi la unyanyasaji katika jamii kwa ujumla - unyanyasaji unafanya watoto kuwa wanyanyasaji.

Kuathirika zaidi: Watoto walionyanyaswa wanakuwa hatarini kudhurika zaidi katika maisha yao ya badaye. Watoto walionyanyaswa kingono, kutelekezwa au walionyanyaswa nyumbani kwao wanaweza kukimbilia mtaani ambapo watakuwa hatarini. Mfano: wasichana waliokimbia nyumbani wanaweza kujihusisha na biashara za ngono au kufanya kazi kama housegirl/houseboy katika mazingira magumu.

Uchumi: Unyanyasaji wa watoto unagharimu fedha - kwa walionyanyaswa, familia zao na kwa jamii yote kwa ujumla. Mifano ya gharama hizo ni: huduma za afya, huduma za kisheria na Ustawi wa jamii, kupunguza kipato kwa aliyeumizwa (shule na kazini).

"Nimefikiria hivi... Mzazi anapompiga mtoto, mtoto hatataka kumwona mzazi tena. Wengine wanatoroka kwa sababu wamepigwa. Mimi niliondoka kwa sababu ya kupigwa."

Mvulana kuhusu kwa nini aliacha nyumbani

"Nilikuwa nakaa na mama yangu mkumbwa, na alikuwa ananinyanyasa. Nilifikiri bora niende sehemu fulani. Lazima nipate mwanaume, niolewe. Nilipoolewa nilikuwa ni miaka 20. Baada ya mwezi moja tu, nilipata mimba - na manyanyaso ya mume wangu yalikuwa mabaya sana. Nilisema, bora niondoke tu."

Mama kijana kuhusu maisha yake

ni kweli kwamba....

Afya mbaya zinazosababishwa na unyanyasaji wa watoto unahusika kwa kiasi kikubwa na mzigo mkubwa wa maradhi duniani. Sasa kuna ushahidi kwamba maradhi makubwa ya utu uzima yana uhusiano na unyanyasaji aliofanyiwa mtu utotoni.
(Source: WHO, 2002)

pia ni kweli kwamba...

Watoto wanaopata adhabu ya viboko wameonyesha kuwa na uwezekano mkubwa kuliko wengine wa kuwa wakatili kwa wenzao; kuonea watoto wengine mashulei; kushiriki katika mienendo isiyo ya kistaarabu wakati wa ujana wao; kuwa wanyanyasaji kwa wachumba zao na watoto wao na kutenda makosa makubwa ya jinai. Serikali nyingi zinaamuru kukomesha adhabu za kikatili kama hatua ya kupunguza ukatili katika jamii.
(Source: Global initiative to end all corporal punishment of children, 2002)

madhara ni yapi?

4.3 Unamtambuaje mtoto aliyenyanyaswa - dalili ni zipi?

Isipokuwa kwa dalili zilizobayana kama majeraha, kuna **dalili za kitabia** zinazoweza kuonyesha kwamba mtoto ananyanyaswa: mtoto anakojoa kitandani usiku, anaanza kuwa mgomvi, kwa ujumla anaonyesha mabadiliko ya kitabia, anaanza kuwa na maendeleo mabaya shuleni, anapenda kukaa mwenyewe na kuwa mwenye huzuni, anaona aibu na kuwa msiri, anapata ndoto mbaya na kukosa usingizi, anaonyesha kutojiamini, anakuwa hapendi kula vizuri, anamkwepa mtu aliyemnyanyasa, anakuwa na wasiwasi, mwili wake haukuwi vizuri.

Inaweza kuwa ngumu kutambua kama mtoto amenyanyaswa kingono, ingawa wanaweza kuonyesha dalili za kitabia zilizo tajwa hapo juu. Kwa kuongeza ni kwamba watoto walionyanyaswa kingono wanaweza kuonyesha dalili hizi: maambukizi sehemu za siri, majeraha sehemu za siri, maumivu ya tumbo chini ya kitovu, kukosa choo, magonjwa ya njia ya mkojo, magonjwa ya zinaa.

unajua kwamba? Tafiti za wanawake katika nchi nane tofauti, ikiwemo **Tanzania**, unaonesha kwamba watoto wanaoishi katika familia zenye migogoro, (ambapo mama alilalamikia unyanyasaji wa kupigwa na baba) walikuwa na uwezekano mkubwa kuwa na matatizo ya tabia kama vile **kukojoa kitandani, ndoto mbaya za usiku** na **tabia za kikakatili**, tofauti na watoto katika familia zisizo na migogoro. Pia, kuna ushahidi kwamba wastani **wa 1/3 ya watoto wachanga wametingishwa** vibaya hata **kufa**, na kwamba wengi wanaonusurika wanaathirika na **madhara ya muda mrefu** kama vile upungufu wa akili, mtindio wa ubongo au upofu (World Health Organization, 2002). Ni dhahiri kwamba, dalili na madhara ya unyanyasaji ni ya uharibifu na yenye kujenga mitazamo ya uhasama/ukatili. Basi fikiria juu ya kinachotokea kulingana na ukweli kwamba, kwa kuwa adhabu ndogo hazina ufanisi, wazazi **wana uwezekano wa kuongeza adhabu** jinsi mtoto anavyokuwa mkubwa. Wazazi wanaotuhumiwa kwa kuwashambulia watoto wao mara nyingi walisema kwamba **ukatili** kwa watoto wao **ulianza kama adhabu ya "kawaida"**. (Source: Global initiative to end all corporal punishment of children, 2002)

4.4 Unyanyasaji unawafundisha watoto nini?

Watu wengi hutumia adhabu ya kiboko kuadabisha watoto. Hata hivyo, mtoto aliyenyanyaswa hata kama ni kidogo tu, anaweza kujifunza yafuatayo:

- Kwamba unyanyasaji ni njia inayokubalika kwa wenye nguvu, wakubwa na wagomvi kupata wanachokitaka kutoka kwa wale ambao ni dhaifu na wenye kupenda amani.
- Unyanyasaji ni njia muafaka ya kutatua ugomvi.
- Kwamba ni muhimu kutumia unyanyasaji kuwafundisha watoto.
- Kwamba mtu anayewapa adhabu - mzazi, mlezi au mwalimu - ni chanzo cha mateso ambacho hupaswa kukwepwa.
- Kumwogopa mtu anayemwadhibu.

"Ukimpiga mtoto anaumia, halafu anakuwa sugu. Kama ameshazoea kupigwa atampiga mwingine."

Mvulana kuhusu unyanyasaji

"Watoto wakinyanyaswa wanakosa kujiamini, ni kama watashindwa kila kitu. Wanakosa raha, wanajidharau."

Mazungumzo ya Msichana kuhusu adhabu za kikatili mashuleni

References

Butchart, Alexander & Harvery, Alison Phinney (2006). Preventing Child Maltreatment - A guide for taking action and generating evidence. World Health Organisation (WHO) & International Society for Prevention of Child Abuse and Neglect (IPSCAN). *Available: www.who.int (as of October, 2008)*

Krug EG et al, eds (2002). World Report on Violence and Health. World Health Organisation. *Available: www.who.int (as of November, 2008)*

Pinheiro, Paulo Sérgio (2006). World Report on Violence Against Children. United Nations. Secretary-General's study on violence against children. *Available: www.violencestudy.org (as of October, 2008)*

Research and Analysis Working Group, United Republic of Tanzania (2008).
Tanzanian Children's Perceptions of Education and Their Role in Society. Views of the children 2007. REPOA on behalf of the Research and Analysis Working Group. *Available: www.repoa.or.tz (as of November, 2008)*

Save the children Sweden (2002). Hitting people is wrong, and children are people too - A practical handbook for organisations and institutions challenging corporal punishment of children. Save the children Sweden. *Available: www.endcorporalpunishment.org (as of September 2008)*

UNICEF (2007). Progress for children - A World Fit for Children Statistical Review. UNICEF. *Available: www.unicef.org (as of October, 2008)*

Edited & designed by Tanja Kisslinger
Photos by Anna Thor

© 2009 Mkombozi

Mkombozi is a registered Tanzania Charity Trust (No. ADP / P12097)

Friends of Mkombozi is a registered UK Charity (No. 1101318)

Kumbukumbu (andika kumbukumbu zako)

Mkombozi ni shirika linaloongoza katika kushughulika na watoto katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha likitumia elimu, utafiti, utetezi na mikutano kuwasaidia watoto wakue kiakili, kiroho na kimwili.

Mkombozi
P.O. Box 9601
Moshi, Tanzania
Moshi tel: +255 27 2754793
Arusha tel: +255 272544319
info@mkombozi.org
www.mkombozi.org
sasa.mkombozi.org